Kilombero mkoani Morogoro, juzi linalomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kikosi cha 837KJ, ikiwa ni ziara yake kutembelea miradi mbalimbali ya jeshi hilo. (Picha na Mpigapicha Wetu).

Serikali kutambua ng'ombe kwa alama za kielektroniki

Dar es Salaam
NA SCOLASTICA MSEWA

SERIKALI imesema imetenga fedha kwa ajili ya kutambua ng'ombe wote nchini kwa kuwaweka alama za kielektroniki ili kuwatambua waliopo na watakaozaliwa.

Pia, imesema mwekezaji wa kuweka alama hizo za kielektroniki amekwisha patikana kwa ajili ya kuanza kuweka alama kwenye ng'ombe.

Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Dk. Daniel Mushi, alisema ng'ombe baada ya kuzaliwa atatambuliwa na serikali kwa kuwekwa alama ambazo zitasaidia kudhibiti wizi wa mifugo kwa kujua ng'ombe huyo yupo wapi na kama amekwisha chinjwa au bado.

Mbali na hilo, Dk. Mushi alisema tayari serikali imetoa mbegu bora za madume ya ng'ombe aina ya borani yenye thamani ya sh. milioni 10 ili kuboresha ng'ombe aina ya zibu wanaofugwa na Wamasai nchini.

Dk. Mushi alisema aina hiyo inayofugwa na Wamasai hawana nyama nyingi na wala hawanenepi kama kama ilivyo kwa aina hiyo ya borani watakao pelekwa wilaya za Kibaha na Mkuranga.

Alisema mbegu za ng'ombe walizopelekewa ni aina inayokuwa kwa haraka na ng'ombe wake hunenepa kwa haraka.

Mushi alisema mbegu bora ya mnyama huchangia katika uzalishaji wa mifugo bora ya wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo hasa katika ukuaji wa mnyama huyo na aina ya nyama atakayotoa.

Alisema nyama nzuri hutokana na aina ya ukoo wa mnyama na mazingira ya mnyama aliyofugwa na upatikanaji wa chakula cha mnyama huyo ili kuongeza tija ya mnyama anayefugwa.

Dk. Mushi akizungumzia uhamasishaji wa mfugaji wa ng'ombe wa mahali pamoja bila kuhamahama, alisema mfugaji anaweza akahifadhi chakula cha mifugo kwa njia za asili kipindi cha miezi miwili mpaka mitatu ambacho kitamsaidia wakati wa kiangazi na kumuongezea kilo kwa unenepeshaji na akapata faida kubwa sokoni.

Alisema mfugo unaotumia muda mwingi kuhamahama na kuzunguka hupoteza muda wa kula, hivyo ni ngumu kunenepa na kukua vizuri.

Scanned with CamScanner

PICHA: MPIGAPICHA WETU

Neema ya bima yaja kwa wakulima, wafugaji, wavuvi

NIPASHE UK8

Na Mwandishi Wetu,
SHINYANGA

WAKULIMA, wavuvi na wafugji wamepatiwa fursa ya bima, ambayo itawalinda dhidi ya hasara.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Jubilee Insurance kuzindua huduma hiyo kuyalinda makundi hayo dhidi ya hasara wanapopata majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri uzalishaji wao.

Bima hiyo ilizinduliwa jana wilayani Kahama mkoani Shinyanga na Mkuu wa Wilaya hiyo, Erasto Kiswaga, katika hafla fupi ambayo pia ilihusisha mafunzo kuhusu umuhimu na faida za bima hiyo kwa wadau mbalimbali wakiwamo wakulima na viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) kutoka mkoa huo.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa wateja binafsi Benki ya NBC, Elibariki Masuke, alisema ujio wa huduma hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kupitia huduma za kibenki zinazolenga kutatua changamoto zinazogusa sekta hiyo muhimu.

"Benki ya NBC tuinatambua vema sekta ya kilimo na zaidi tunatambua mchango wa wakulima katika uchangiaji wa uchumi wa nchi na kwa msingi huu tumeona ni vema kuja na bima ya mazao kwa wakulima. Bima hii ni ya kwanza nchini na tunaamini kwa dhati kwamba kupitia bima hii wakulima watapunguza kwa kiwango kikubwa hasara zitokanazo na majanga mbalimbali yasiyotabilika yaani yale yalio nje ya uwezo wao." alisema.

Alisema ujio wa huduma hiyo utawasaidia Watanzania ambao asilimia 70 wanategemea shughuli ya kilimo kwa kuwapatia uhakika wa matokeo wanayoyatarajia kupitia shughuli zao za kilimo, uvuvi na ufugaji hata pale wanapokabiliwa na majanga ya asili ikiwamo mvua ya mawe, mafuriko, ukame, upepo mkali, moto na majanga mengine ambayo yamekuwa yakiwasababishia hasara kubwa na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Kiswaga alitoa wito kwa wakulima hao kutumia fursa hiyo kukata bima ili iwasaidie kuwakinga wanapokumbwa na majanga mbalimbali, huku akiitaja sekta ya kilimo kuwa miongoni mwa sekta zinazokabiliwa na majanga mengi yasiyotabirika ikiwamo mafuriko, moto, wadudu na ukame ambavyo vimekuwa vikiwasababishia hasara kubwa wakulima.

"Hizi ni dalili njema kuona sasa huduma za bima zimeanza kuwafikia wakulima ambao kimsingi ndio kundi kubwa zaidi katika shughuli za uzalishaji hapa nchini likigusa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania. Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wa vyama vya msingi mliohuduhuria uziunduzi huu vipeleke mpango huo kwenye bodi za mazao mbalimbali ili utaratibu wa kuwalipia bima hii wakulima uanze mara moja,"

Awali akifafanua zaidi kuhusu huduma hiyo, Mkuu wa Idara ya Bima wa Benki hiyo, Benjamini Nkaka, alizitaja bima hizo kuwa ni pamoja na bima ya mazao inayohusisha mazao yote ya chakula na biashara pamoja na mazao ya matunda, bima ya mifugo inayohusisha mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi kondoo pamoja na Bima ya samaki mahususi kwa ajili ya wavuvi.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima hao Mwenyekiti wa Chama Kikuu la Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema huduma hiyo imekuja wakati mwafaka katika kipindi ambacho wakulima wamejipanga kufanya mapinduzi ya kilimo kupitia kilimo cha kisasa kinachoshusisha tahadhari zote muhimu ili kuepuka hasara ambazo zimekuwa zikiwarudisha nyuma kimaendeleo.

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 8.

RC awaasa watendaji migogoro wakulima na wafugaji

Na John Gagarini, Kibaha

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (pichani) amesema atawawajibisha watendaji wataalamu au viongozi ambao wanaonekana kuwa ni sehemu ya migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa kero kubwa kwa sasa kwenye mkoa huo licha ya sheria kuwepo.

Aidha, amesema viongozi na watendaji hao wanazo njia mbili, ama kutatua migogoro hiyo au kuachia ngazi.

Alisema hayo Mjini Kibaha wakati wa mkutano wa mashauriano kuhusu mpango wa kukabiliana na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kwa kutumia mfumo wa ranchi ndogo kwenye mkoa huo.

Kunenge alisema haiwezekani migogoro iendelee ilhali viongozi wapo na sheria zipo.

"Hakuna kitu kinachonipa changamoto kama migogoro ya wakulima na wafugaji, lazima watu waishi pamoja wakulima na wafugaji wote muhimu tunategemeana, inapotokea migogoro athari zake ni mbaya kwa wananchi, wakati mwingine maisha ya watu yanapotea, hatuwezi kuendelea hivi, sisi watumishi wa wananchi tunapaswa kuwaondolea kero hizo," alisema.

Alisema: "Baadhi ya viongozi ambao wanapaswa kutatua migogoro hii wamekuwa wakiwapa watu namba yangu ya simu ili wanipigie badala ya kuitatua, hali ambayo sitaikubali

tutawajibishana kwenye hili, kama wewe ni kiongozi kwa nini ushindwe kufanya utatuzi ilhali sheria mnazo."

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Abdallah alisema migogoro hiyo imekuwa kero kubwa kutokana na baadhi ya wafugaji kutumia fedha kuhonga kwenye baadhi ya maeneo, hali ambayo inasababisha migogoro hiyo kutokwisha.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete alisema baadhi ya wafugaji wavamizi ndio chanzo kikuu cha migogoro hiyo.

Ridhiwani alisema sheria inataka wafugaji wanapotaka kuingia sehemu lazima watoe taarifa kwenye vijiji. "Lakini wavamizi hao huwa wanaingia kinyume cha sheria hiyo," alisema.

Kwa mujibu wa Ridhiwani, kwa Halmashauri ya Chalinze, kuna vijiji vitano vilitengwa kwa ajili ya wafugaji na ndiko wanakokaa wafugaji wenyeji na wamekuwa wakiishi kwa amani bila ya migogoro.

Scanned with CamScanner